## UFUNDISHAJI UNAOZINGATIA MATOKEO YA UPIMAJI:

# Ngazi ya darasani

## Utangulizi na Kusudi

Kutumia upimaji katika kufundisha ni mkabala wa lazima katika kuimarisha ubora wa ufundishaji ili kuongeza uwajibikaji wa ujifunzaji kwa mwanafunzi na kuhakikisha uimarishaji zaidi unaozingatia usawa katika uimarishaji wakati wa utendaji.

Upimaji unapojumuishwa wakati wote wa ufundishaji hutumika kama kipimo na utaratibu kwa ajili ya ubora, uwajibikaji, na usawa katika darasa. Kama kipimo, upimaji unaweza kusaidia kutujulisha: Je, malengo ya kujifunza yamefikiwa? Je, wahusika wa darasa (wanafunzi, walimu, walimu wakuu, wanasihi elekezi) wanaendeleza jukumu lao katika kufika matokeo ya kujifunza yaliokusudiwa? ujifunzaji unafanyika kwa wanafunzi wote au ni wachache waliochaguliwa? Upimaji unapotumika kama utaratibu, unaweza kusaidia kuwezesha ufundishaji wenye ubora wa hali ya juu kwa kutoa taarifa zenye kujali muda kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Upimaji unapotumika kwa ajili ya kujenga, matokeo yake huwasaidia wanafunzi, walimu, wanasihi elekezi na walimu wakuu kuwajibishana ili kufikia malengo ya kujifunza. Pia (matokeo hayo) yanaweza kuwasaidia walimu kufanya marekebisho na mbinu za kufundishia. Upimaji ni muhimu kwa kuendeleza ufundishaji ulioimarika kwa kutayarisha andalio la somo, matumizi ya zana za kufundishia, na mikakati ya kufundisha, pamoja na mafunzo ya ualimu na usaidizi endelevu. Vile vile unaweza kutumiwa kuongeza usawa iwapo utatumiwa kuanisha kwa uratatibu, na kushughulikia mahitaji ya kujifunza kwa mwanafunzi mmoja mmoja au kikundi.

**Kielelezo Na. 1. Malekezo ya Jumla kuhusu Ufundishaji unaozingatia matokeo ya Upimaji**

**UPIMAJI KATIKA MFUMO**

*Angalia Ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji: Mwongozo katika hatua*

Kipimo cha ufundishaji na matokeo ya kujifunza katika ngazi mbalimbaliza mfumo wa elimu

**UPIMAJI NDANI YA DARASA**

*Yaliyomo kwenye mwongozo huu*

Upimaji unaotumika kuleta mabadiliko ya mtaala au ufundishaji

**UPIMAJI ENDELEVU**

Upimaji wa muda maalum **Muda maalum katika kalenda ya masomo au muda maalum katika utekelezaji wa afua**

Upimaji wa wakati maalum katika kalenda ya masomo **Kupima maendeleo ya wanafunzi na lengo la kujifunza**

**UPIMAJI KWA AJILI YA KUJIFUNZA** (AFL)

Mchakato ambao upimaji endelevu hutumika wakati wote na kubadilisha ufundishaji.

Upimaji wa mwisho unaweza kuwa endelevu kama unatumika kuongoza hatua za baadae za ufundishaji, au kurekebisha nyenzo na msaada kwa walimu au wanafunzi

**UPIMAJI WA UJIFUNZAJI**

Mchakato wa kutumia upimaji wa mwisho kutathmini maarifa na utendaji kwa kuzingatia malengo ya mtaala yanayofuatiliwa kupitia tathmni kwa ajili ya kujifunza na tathmini kama kujifunza. Inaweza kutumika kwa kupanga mpango wa siku za usoni na tathmini binafsi ya mwalimu

**UPIMAJI TAMATI**

Upimaji unaotumika **kujulisha na kurekebisha uandaaji wa afua pamoja na mtaala, mafunzo na usaidizi endelevu kwa walimu**

Upimaji unaoendelea rasmi na usio rasmi kuangalia **uelewa wa wanafunzi na ujifunzaji**

**UPIMAJI KAMA KUJIFUNZA**

Mchakato wa kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi kutumia upimaji endelevu kuona maendendeleo yao na kutafakari juu ya ujifunzaji wao

*Masharti yaliyo hapo juu ni maarufu katika fasihi iliyopo juu ya tathmini na wakati mwingine hutumiwa kwa kubadilishana au kwa njia zinazoingiliana. kielelezo ulio hapo juu unaonyesha istilahi zitakazotumika katika mwongozo huu. Maneno haya yamefafanuliwa zaidi, kwa mifano, katika sehemu zifuatazo.*

*Kupima kujifunza, kupima kama kujifunza na kupima kwa ajili ya kujifunza ni istihahi ambazo zipo ngazi ya mfumo. Hata hivyo kwa makusudio ya mwongozo huu tu- nazijadili istilahi hizo katika mkutadha wa darasani kama zilivyoainishwa kwene kielelezo hapo juu.*

Ufundishaji wa darasani unaozingatia matokeo ya upimaji unatakiwa uzingatie mfumo mpana wa upimaji unaotumika kukusanya taarifa kuhusu mwanafunzi anavyojifunza, kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi na kutoa taarifa kwenye ngazi ya mfumo wa maamuzi.Mfumo huu mkubwa wa upimaji unajumuisha upimaji unaofanywa kupitia skuli au mitihani ya wilaya kupitia upimaji wa kiwango kikubwa kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa mfumo. Mwongozo huu unajikita kuangalia ni kwa namna gani watunga sera, wafadhili na wadau wa utekelezaji wanaweza kuimarisha ufundishaji unaotokana na tathmini ndani ya darasa, hususan katika maeneo ambayo walimu wanahitaji usaidizi katika kuingiza upimaji katika kufundisha. Mwon- gozo huu unatoa usaidizi kwa walimu namna mbinu ya ufundishaji unaotokana na upimaji unaweza kutekelezwa kwa namna ambayo hautakuwa mzigo kwa walimu na kuonekana kuwa ni kazi ya ziada katika kufundisha. Ufundishaji unaotokana na upimaji: *Mwongozo katika ngazi ya Mifumo* unafafanua upimaji katika hatua nyenginengine za mfumo.

## MPANGILIO


Mwongozo huu umeandaliwa kama ifuatavyo: Kwanza, unajadili maana ya ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji, unaeleza kiini cha dhana ili kufahamu aina ya ufundishaji ndani ya darasa na kuelezea baadhi ya changamoto wanazozipitia walimu katika nchi zenye kipato cha chini na cha kati. Pia inaeleza namna ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji unaweza kutekelezwa na walimu, namna walimu wanaweza kupima kwa ajili ya kujifunza. Mwisho, unatoa mfululizo wa mapendekezo ya namna ya kutoa usaidizi kwenye ufundishaji unaotokana na upimaji kama sehemu ya hatua ya msingi ya kusoma na kuhesabu.

## MAANA YA UFUNDISHAJI UNAOZINGATIA MATOKEO YA UPIMAJI?

Ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji unamaanisha shughuli zinazofanywa na walimu na wakati mwingine wanafunzi, na washauri wa walimu ambao hutoa taarifa kwa wakati ili kujua maendeleo na kurekebisha shughuli za kufundisha na kujifunza zinazokuja.Kama ilivyooneshwa katika kielelezo Na. 2, shughuli hizi hutafauatina kwa muda, kujirudia na muundo kutoka kwa uchunguzi wa dakika namna mtoto anavyosoma hadi kwenye zoezi la kila wiki la tahajia za neno au kazi mradi kuhusu kuongeza na kutoa vihesabio katika ghala ya kuigiza. Upimaji wa mwisho na ule wa muda wote unaweza kutumika kuonesha ufundishaji, kutegemea kama lengo lililokusudiwa katika mchakato wa kufundisha na kujifunza limefikiwa. Upimaji wa kujifunza hutusaidia kutujuilisha njia sahihi ya kufikia lengo la kujifunza (Upimaji kwa ajili ya kujifunza).

**Ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji unatakiwa ndio uongoze ufundishaji kwa uhalisia.** Sio uchunguzi unaosimama peke yake au upimaji tamati. Wala sio mchakato unaolenga kubainisha wanafunzi wanaojifunza kwa shida. Ufundishajii unaozingatia matokeo ya upimaji unalenga kweye ufanisi wa kasi ya mwalimu na ufundishaji, na ukitumika kama unavyostahiki unaweza kubaini mafanikio na mapungufu ya kujifunza kwa kila mwanafunzi na kisha kuwasaidia walimu kufundisha vizuri.

### KUTANA NA MWALIMU DEE




Mwalimu Dee anafundisha darasa la 2 katika skuli iliyo mbali na miji mikubwa lakini yenye mwonekano mzuri wa milima. Skuli yake ina bustani nzuri na iko karibu na mji wa kibiashara usio na umeme.

Katika darasa lake Mwalimu Dee ana vitabu vya kusoma na kuhesabu vilivyoandikwa katika lugha mama, pia vihesabio vya mfuniko wa chupa na vibao 60 kwa ajili ya wanafunzi wake. Mwalimu Dee anaipenda kazi yake na wanafunzi wake pia. Amefanya hivyo kwa miaka 15 sasa! Hata hivyo bado anakabiliana na changamoto za kujifunza. Ni theluthi moja ya wanafunzi wake watakuwa na stadi za awali za kusoma na kuhesabu ifikapo mwisho wa darasa la 3

*Kwa kutumia mfano wa Mwalimu Dee, onyesha namna ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji unaweza kufanyika katika mazingira yenye raslimali chache. Mwangalie Mwalimu Dee na utafute suluhisho kupitia mwongozo huu!*

Pengine sehemu muhimu sana na yenye changamoto kwenye ufundishaji unaotokana na upimaji**, ni kuwasaidia walimu kuchukua hatua zinazostahiki katika kutafuta majibu ya taarifa zilizopatikana kupitia taarifa zilizokusanywa wakati wa upimaji**. Hii ni hatua muhimu sana, kwa sababu ni sehemu ya fumbo ambalo linaaweza kushawishi ujifunzaji na ufundishaji. Upi- maji unakuwa na maana pale walimu wanapoona matumizi ya upimaji katika kufundisha yanawasaidia wanafunzi kujifunza na hatimaye wanafunzi kuthamini na kutumia uzoefu huu zaidi katika ujifunzaji.

**KIELELZO NA. 2 . Upimaji wa Mfano wa Ufahamu**




## UPIMAJI WA KUJIFUNZA

Upimaji wa kujifunza (UwK) darasani unamaanisha matumizi ya upimaji tamati unao- fanyika kila mwisho wa muda wa kujifunza, kama ilivyo kwenye mtaala, au muda maalum kama vile mwisho wa muhula. UwK una lengo la kuangalia nyuma kuona maeneo ambayo wanafunzi wamefanikiwa kwa kulinganisha na malengo ambayo mwalimu amekuwa akiyafuatilia kipindi chote cha somo kwa mwaka husika. Upimaji tamati unatakiwa uoneshe ufundishaji na kujenga uzoefu wa kujifunza wenye usawa badala ya kuwaadhibu wanafunzi wanaonekana kuwa nyuma wakati wa kujifunza. Wanatakiwa walinganishwe kwa namna ile ile na upimaji uliofanywa mwanzo wa mwaka ili kusaidiwa kuweka malengo kwa somo linalofuata, kuonesha matarajio ya mtaala na kuwapa walimu nafasi ya kufanya tathimini binafsi ya mbinu iliyofanikiwa.

## TATHMINI YA KUJIFUNZA

Upimaji kwa ajili ya kujifunza mara nyingi ni upimaji usio rasmi,endelevu, unaofanya tathmini ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani. Lengo kuu ni kushauri marekebisho yanay- ofaa ya ufundishaji ili kuleta mabadiliko yenye manufaa. Upi- maji na ufundishaji ni sehemu ya mzunguko wa ndani wa kuinua ujifunzaji wa mwanafunzi. Walimu wanatakiwa kupima ujifunzaji mara kwa mara kuweza kufahamu kiwango cha mwanafunzi katika kufikia lengo la kujifunza na njia sahihi ya kufikia lengo la kujifunza. Upimaji endelevu na Upimaji tamati unaweza kutumika kupima kwa ajili ya kujifunza. Ila muundo na kujirudia rudia kwa upimaji endelevu ambao umo ndani ya mchakato wa kujifunza au kama uangalizi wa uelewa unaojirudia rudia inatoa tafsiri kuwa upimaji endelevu ni upi- maji rahisi unaotumika mara nyingi kwa ajili ya kusudi hili (An- galia jedwali la kwanza)

### UPIMAJI WA MWALIMU DEE

Mwalimu DEE amealikwa kuhudhuria mafunzo katika ngazi ya wilaya kuhusu utumiaji wa upimaji kwa ajili ya kujifunza. Katika maisha yake hajawahi kusikia kuwepo kwa shughuli kama hii. Mwalimu Dee hufundisha kwa ajili ya kuwasaida wanafunzi wake wafaulu mtihani wa taifa wa ufahamu ili waweze kuvuka kwenda darasa la 3. Mwalimu Dee huwaita wanafunzi walio mbele na nyuma, na wakati mwingine huwaweka katika jozi. Pia huwaambia wafanye hesabu kwenye vibao vyao vya kuandikia na baadaye waandike kwenye madaftari yako wakati anawakagua. Hata hivyo, Mwalimu Dee amefundishwa kufuata mwongozo wa mwalimu wa kusoma na kuhesabu ulio kwenye lugha mama.

Mwalimu Dee hajui atabadilisha nini katika ufundishaji kuhusu kazi halisi za wanafunzi.

Upimaji kwa ajili ya kujifunza ni mkakati muhimu kwa sababu sunatengeneza fursa ya kukumbuka, kukazia na kutumia stadi na uelewa wa maudhui kila wakati katika msingi wa stadi ya kusoma na kuhesabu. Msingi wa stadi za kusoma na kuhesabu huwasaidia wanafunzi kujenga stadi hizi muhimu ( sauti ya herufi na ubainishaji wa namba) kisha kwenda kwenye hatua ngumu (ufahamu na kujua maswali na kujibu majibu ya kuhesabu yenye kuhitaji hatua anuai.) Upimaji edelevu, unaweza kuongeza kiwango cha juu cha kufikiri kama utatoa changamoto kwa wanafunzi kufanya tafakari binafsi kuhusu ujifunzaji wao na kushiriki kwenye upimaji rika. Kuna ushahidi kuwa Upimaji imara kwa ajili ya kuiifunza unaweza kuwa na matokeo makubwa nakuimarisha matokeo ya ujifunzaji miongoni mwa wenye changamoto za kujifunza.[10]

Ufundishaji unaozingatia matokeo ya Upimaji kwa mujibu wa Mtandao wa Kusoma wa Dunia: Andiko kuhusu upimaji endelevu linafafanua kwa undani kuhusu upimaji endelevu.

Wataalam wengi katika eneo la upimaji kwa ajili ya kujifunza, wanaamini kuwa kama upimaji huu ukifanyika vizuri unaweza kuwa na mafanikio makubwa katika Upimaji wa Utendaji wa Kimataifa kwenye nchi za Kaskazini [11] na kuwa na manufaa zaidi katika nchi zenye uchumi mdogo na wakati.[12] Matokeo haya

yanategemea na urahisishwaji wa utendaji kwa wallimu, kutoa usaidizi ili watumie mbinu hii mara kwa mara na kutafautisha matokeo ya upimaji, pia kuhamasisha mazingira ili upimaji uonekane kuwa una lengo la kusaidia na sio kuogopesha [13].

## UPIMAJI KAMA UJIFUNZAJI

Upimaji kama Ujifunzaji (UkU) unafanya kazi kama ukamilisho wa mchakato ambapo wanafunzi wanatumia ujifuzaji wao binafasi au wao kwa wao, kutengeneza fursa kwa ajili ya tafakari binafsi na umiliki. UkU unaanza kwa mwalimu na mwanafunzi kuweka lengo la kujifunza, na kisha wanafunzi wanaongoza mchakato wa kufuatlia maendeleo ya kujifunza ili kufikia lengo walillokubaliana. Kwa mfano wanafunzi wanaweza kusahihisha maswali ya Hisabati na kujadiliana makosa yanayofanana, kusoma insha ya kila mmoja na kisha kupeana maoni na mrejesho. Mbinu hii imethibitika kuongeza hali ya kujiamini kwa wanafunzi [14], kujitambua na ujifunzaji tenda.[15] Mbinu na shughuli za UkU zinatakiwa ziendane na makuzi ya utambuzi, kijamii na kihisia ya mwanafunzi wakati wa elimu ya awali na kujumuisha na mbinu ta- fauti kama UkU ile zenye kuzingatia kuwa mwanafunzi ndio anachukua jukumu la kujipima na wala sio mwalimu. Ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anafaidika kwa usawa, mwalimu awasaidie wanafunzi kwa kuwaeleza vizuri wana- funzi malengo ya upimaji, matokeo yanayotarajiwa, vigezo vya kuweka alama na kuvipanga vigezo husika kutokana na uwezo tafauti wa kujifunza wa mwanafunzi.[16] Kutokana na muingiliano wa UkK na UkU, mwongozo huu unatambua aina zote mbili za upimaji kama ni Upimaji kwa ajili ya Kujifunza.

**Jedwali Na. 1. Upimaji kwa ajili ya Kujifunza dhidi ya Upimaji wa ujifunzaji**

| | AINA YA UPIMAJI | ENDELEVU AU TAMATI? | MIFANO KATIKA KUSOMA | MIFANO KATIKA KUHESABU |
|---|---|---|---|---|
| **Upimaji kwa ajili ya Kujifunza na Upimaji kama Kujifunza (UkwK na UkU)** | Matendo wakati wa kufundisha | **Endelevu:** Wakati wa kujifunza, mwalimu anawapima wanafunzi kama wanajifunza kwa vitendo stadi na kutoa msaada inapobidi. | Katika jozi wanafunzoi wanajifunza kuunganisha sauti za herufi na wenzao na kupeana mrejeho wakati mwalimu akichunguza na kutoa msaada. | Wanafunzi "wanaonyesha na kusema", kujumlisha namba katika vibao wakati mwalimu akiwa anak- agua na kutoa msaada |
| | Uchunguzi wenye ushahidi wa simulizi | **Endelevu:** Mwalimu anapima huku anaandika nukuu kwa ajili ya rejea yake kuhusu kazi ambazo wanafunzi wanazimudu na zile ambazozinawapa changamoto. *Kisha anawapanga katika jozi kulingana na uchunguzi wake.* | Mwalimu anasoma hadithi kwa sauti kisha anauliza maswali kabla, wakati na baada ya kusoma ili kujua ni nani anayeweza kujibu maswali kwa ufasaha anapowaita. | Mwalimu anaandika kumbukumbu wakati wa shughuli na wakati huo wanafunzi wanapanga vitu kwa ukubwa. |
| | Kusahihisha daftari | **Endelevu:** Mwalimu anapitia na kusahihisha madaftari ya wanafunzi. *Anarudia kufundisha maeneo ambayo yana mapungufu* | Mwalimu anapitia insha waliyoandika Wanafunzi wa darasa la 3 kwenye kusoma na kutoa nafasi *kwa wanafunzi kufanya marudio ku- tokana na mrejesho aliowapa.* | Mwalimu anasahihisha zoezi la nafasi ya thamani ambayo wanafunzi wamemaliza na kuzungushia duara *zile ambazo wamekosa kwa ajili ya kurudia na kusahihisha.* |
| **Upimaji wa ujifunzaji (UwK)** | Jaribio la wiki | **Tamati:** Mwisho wa wiki, mwalimu anapima kama wana- funzi wamemudu stadi za msingi za kusoma na kuhesabu alizofundisha wiki iliyopita. *Anaandaa mpango kwa wanafunzi wanaohitaji msaada wa ziada..* | Wanafunzi wanasoma aya fupi au orodhe ya maneno yanye herufi walizosoma wakati wa kipindi *Wanafunzi ambao wameshindwa kusoma walau vipengele vitatu kati ya vitano, mwalimu anawasahuri wahudhurie kwenye klabu ya kusoma kwa dakika 20 mpaka30 baada ya masomo kwa siku hiyo.* | Wanafunzi wanapewa zoezi la kujumlisha nambari zenye tarakimu moja kwa kutumia vitu halisi. *Wana- funzi wanaopata chini ya saba kati ya 10 wanapewa msaada wa ziada kutoka kwa mwanafunzi mwenye ufahamu zaidi au mwalimu* |
| | Jaribio | **Tamati:** Mwisho wa mtiririko wa somo, muhula au darasa, mwalimu anawapa jaribio la kuandika au la kuzungumza kupima kama wanafunzi wameweza kumudu lengo lilotarajiwa. *Baada ya hapo mwalimu anaandaa mpango kwa wana funzi wenye mahitaji zaidi au shughuli yenye changamoto zaidi kwa wanafunzi.* | Wanafunzi wanasoma matini fupi kwa kutumia misamiati iliopo kwenye matini kwa usahihi, kisha wanajibu maswali yanayoendana na kifungu walichosoma. | Wanafunzi wanamaliza zoezi la vipimo linalooana na mada walilofanya kwenye kipindi kilichopita |

Ushahidi unathibitisha kuwa ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji kupitia UkwU una ufanisi zaidi katika kuimarisha matokeo ya KKK hasa kama kile kilichofundishwa na kupimwa kimejumuisha uwezo wa wanafunzi, mahitaji na malengo ya kujifunza.[17] Bila shaka upimaji kwa ajili ya kujifunza unaimarisha matokeo pale ambapo walimu wanaweza kutenda,

kuchanganua na kutafsiri matokeo yanayotokana na upimaji, na hii ndio sababu programuu ya KKK haitakiwi kuwa na matarajio makubwa kuhusu hizi shughuli ambazo ni ngumu na zenye mfumo wa kikanuni. Kielelezo Na. 3 kinafupisha kanuni nne zinazojitokeza kwenye mikabala iliyofanikiwa kwa KKK, na kuwekwa katika kumbukumbu na RISE kama kanuni za Ngazi za Kuimarisha Ufundishaji zenye Malengo na Mahitaji kwa Wanafunzi (NKUMMW)[18]. Kanuni hizi zinapaswa zitumike kwa uundwaji wa afua za KKK zenye ubora wa juu.

Licha ya kukubalika kwa manufaa ya matumizi ya Upimaji kwa ajili ya Ujifunzaji19, jinsi ya kutumia upimaji endelevu imethibitika kuwa na ugumu sana miongoni mwa walimu na mifumo katika maeneo mbali mbali.20 Ni vizuri ifahamike kuwa ugumu huo sio kosa la walimu bali ni utaratibu usiofaa wa kutengeneza programu ambazo huunda programu zisizoendana na hali halisi ya darasani katika nchi zenye uchumi wa chini na wa kati. Mara nyingi sio uhalisia kulinganisha maamuzi halisi ambayo walimu hulazimika kuyafanya kila sikukatika mukhtadha wa kufanya afua fanisi za KKK.

Zifuatazo ni changamoto nne za msingi katika kutekeleza upimaji kwa ajili ya ujifunzaji. Baada ya hapo tutaangalia njia zinazofaa kukabiliana na changamoto za kutekeleza mbinu ya upimaji kwa ajili ya ujifunzaji.

**KILELEZO NA. 3. Kanuni za NKMMW**

**Kanuni 1:** Weka malengo ya kujifunza yanayoshabihiana na ngazi ya wanafunzi ya kujifunza.

**Kanuni 2:** ufundishaji ushabihiane na ngazi ya wanafunzi ya kujifunza na lengo la maendeleo ya kujifunza.

**Kanuni 3:** Kutoa msaada wenye tija na mantiki kwa walimu

**Kanuni 4:** Tafuta njia ya kutekeleza kanuni zili- zotangulia kutegemeana namazingira yanayokuzunguka.


**1. Kujua unapima nini na lini:** WKama upimaji haukuingizwa moja kwa moja kwenye kiongozi cha mwalimu au kitabu cha mwanafunzi, walimu wanalazimika kupanga ni wakati gani wa kufanya upimaji na kuandaa mfumo wao wa upimaji. Hata hivyo, walimu watatakiwa kupata mafunzo kabilishi na msaada katika kuzibaini fursa za kufanya upimaji usio na tija.

**2.Kutenga muda unaohitajika kufanya upimaji na marekebisho:** Katika mazingira tafauti walimu wanahisi kuwa muda wa kufundisha kusoma na kuhesabu hautoshi kuendanda na mtaala, na muda ni mdogo zaidi kwa ajili ya kufanya upimaji, mapitio na marekebisho. Pia baadhi ya walimu wanaamini kuwa kufundisha darasa lenye wanafunzi wengi linafanya upimaji wa wanafunzi, kutafsiri matokeo na kufanya marekebisho ya ufundishaji kulingana na matokeo ya upimaji kuonekana ni mchakato unaochukua muda mrefu. Walimu wanahitaji msaada namna ya kuweza kutumia mbinu hizi wakiwa na furaha na bila kutumia muda mwingi.

**3.Kutunza kumbukumbu na kufuatilia matokeo ya upimaji:** Ugumu sio kuwapima wanafunzi tu ila hata kufuatilia maendeleo yao kwenye darasa la wanafunzi wengi inakuwa ni chagamoto kubwa hasa katika mazingira ambayo mwalimu hana utamaduni wa kutunza kumbukumbu za kila siku.Utunzaji wa kumbukumbu huhitaji baadhi ya vifaa kama vile kalamu, bahasha na vishikwambi ambavyo vinaweza visipatikane kwa urahisi. Baadhi ya mbinu za ufuatiliaji zimekuwa zikipoteza maana kutokana na urasimu na mlolongo mrefu wa utawala ambao huonekana kuwa mzigo kwa mwalimu. Ni vizuri tukafahamu kuwa, ufuatiliaji wenye mafanikio hauhitaji mwalimu kumfuatilia kila mtoto kila wakati anapofanya upimaji.

**4.Kutumia matokeo:** Jambo muhimu zaidi kwa walimu ni kutumia matokeo, lakimni walimu wanaweza kuhisi ama hawajui jinsi ya kutumia matokeo au hawana rasilimali za kutoa msaada wa marekebisho au shughuli za ziada ambazo zinaweza kuhitajika. Wakati ambapo upangaji wa ufundishaji ambao walimu wanahitajika kufanya kwa kuzingatia matokeo ya upimaji unaweza kuwa mpana (unajumuisha mbinu mbali mbali za ufundishaji na kutumia program u ya marekebisho ya ufundishaji), kuanzisha njia japo rahisi za kutumia matokeo ya upimaji inaweza kuongeza utumiaji kwa mwalimu.

**MWITIKIO WA MWANZO WA MWALIMU DEE KUHUSU WAZO LA UPIMAJI**



""Hapa tunaendelea tene na mikabala mipya ya ufundishaji. Hivi hawa watu wanafikiri nina muda kiasi gani? Wamewahi kufundisha darasa la wanafunzi 60 wenye umri wa miaka 8 ndani ya darasa moja? Inanichukua dakika 10 kuita majina, dakika 20 kugawa vitabu na kuhakikisha kila mtoto yuko katika ukurasa unaotakiwa (kwa sababu theluthi moja ya wanafunzi jana hawakuja skuli), na ninahitaji masaa 2 hasa wakati wa usiku kusahihisha madaftari za wanafunzi kwa kutumia taa yangu ndogo inayotumia nishati ya jua. **Tazama,na sasa naambiwa kuwafuatilia jinsi wanafunzi wote 60 wanaendeleaje dakika baada ya dakika**

Kilichobakia katika mwongozo huu kimsingi kinalenga upimaji kwa ajili ya kujifunza kwa sababu ni kiini cha kuimarisha matokeo ya KKK katika nchi zenye Uchumi wa chini na Uchumi wa Kati ambapo hadi sasa uko chini ya kiwango ukilinganisha na UwU. Majadiliano yanayofuata yanatupa mikakati ya kukabiliana na changamoto nne za msingi za kutekeleza Upimaji kwa ajili ya Ujifunzaji kama ilivyoelezwa hapo juu.

# Walimu wanapimaje ujifunzaji?

Wakati wa kuandaa shughuli za upimaji kwa ajili ya ujifunzaji darasani, walimu wanatakiwa wajiulize wenyewe maswali manne ya kuwaon- goza[21]:

Mbinu ya Kufundishaia katika Ngazi Sahihi (TARL) iliyoasisiwa na Pratham na J-Pal inalenga kuwasaidia walimu kutumia taarifa za upimaji endelevu:

"Kwa kumpima mtoto mmoja mmoja, mwalimu anaelewa mahitaji ya kujifunza kwa kila mtoto. Mwalimu anatumia matokeo ya upimaji kutengeneza kikundi anachoweza kukisimamia chenye watoto wenye mahitaji ya kujifunza yanayofanana. Matokeo ya taarifa za upimaji humsaidia mwalimu kuandaa shughuli stahiki zenye lengo la kuwasaidia watoto kujifunza. Mchakato wa upimaji unawapa nafasi walimu na washauri kufuatilia ufanisi na kusaidia mfumo mzima kuweka mkazo kwenye maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji"[22]

1. Kwa nini ninapima?
2. Ninapima nini?
3. Mbinu zipi za upimaji natakiwa kuzitumia kukusanya ushahidi wa ujifunza ji wa wanafunzi
4. Nitazitumia kwa namna gani taarifa nilizozikusanya katika upimaji wangu, na nitafanya hivi lini?

Waalimu watakuwa na uwezo tafauti namna ya kuyajibu maswali haya na kutumia ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji. Ni jambo jema kuwaona walimu wakianzia kwenye hatua ya awali ya kutumia upimaji wa darasani (ngazi ya kwanza) kisha kwenda kwenye hatua ya juu na matumizi ya kiwango cha juu ya matumizi ya matokeo ya upimaji ikiwa ni pamoja na maswali ya kufikiri ya ngazi ya juu kwa ajili ya ku- panga ufundishaji (**ngazi ya 4**) kama ilivyooneshwa kwenye **jedwali la 2**. Ni muhimu kukumbuka kuwa programuu za KKK mara nyingi huwalenga walimu ambao wanahitaji msaada kama ulivyooneshwa kwenye ngazi ya 1 au ya 2. Kwenda katika hatua ya mbele inahitaji mi- aka kadhaa ya kusaidiwa. Ni matarajio yasiyo na uhalisia kuwa na pro- gramu ya kusaidia walimu kuwatoa kwenye ngazi ya 3 kwenda ya 4 wakati walimu walio wengi wako katika ngazi ya chini. Kwa hivyo, ni muhimu kuweka lengo la kusaidia walimu kulingana na ngazi yao halisi.

**Jedwali la 2.** Mwendelezo wa Upimaji kwa ajili ya kujifunza ndani ya darasa.

| | JINSI INAVYOONEKANA DARASANI | MFANO | MSAADA SAHIHI WA KUHIMIZA NA KUMPELEKA MWALIMU NGAZI INAYOFUATA |
|---|---|---|---|
| **Ngazi ya 1:**Msingi | Mwalimu anazunguka darasani akichunguza na kutoa msaada kwa wanafunzi. | Mwalimu anaonesha vidole vya wana- funzi kwenye maneno wanayotakiwa kuyasoma. Wanasahihisha madaftari ya mazoezi kwa kuweka alama ya vyema na x bila kuweka kumbukumbu. | **Kuwa na shauku na kujiamini**<br>**Vifaa:** Michezo ya Upimaji endelevu, rahisi na yenye kufurahisha inaweza kujumuisha chati rahisi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za matokeo (kwa mfano, *"Kidole gumba juu/kidole gumba chini, -hesabu wanafunzi wangapi wamepata jibu sahihi)."*)<br>**Mafunzo:** Wakufunzi hujihusisha na walimu kupitia michezo ya tathmini ya kufurahisha na maonyesho kutoka kwa walimu "bingwa".<br>**Usaidizi endelevu kwa walimu:** Wanasihi elekezi huwauliza walimu kushiriki katika "onyesha na eleza" ambapo wanawaonye- sha wenzao jinsi walivyozoea mchezo wa tathmini kwa darasa lao. Wanasihi elekezi wakiwatembeza walimu kutathmini kikamilifu idadi ndogo ya wanafunzi na kurekodi na kujadili habari. Walimu wanabadilishana uzoefu"kujaribu" mbinu tofauti za tathmini katika Jumuiya iliyoongozwa Majadiliano ya Mazoezi. |

| | JINSI INAVYOONEKANA DARASANI | MFANO | MSAADA SAHIHI WA KUHIMIZA NA KUMPELEKA MWALIMU NGAZI INAYOFUATA |
|---|---|---|---|
| **Ngazi ya 2:** Kukuza mazoezi | Mwalimu anasaidiwa katika kutumia upimaji rahisi na fomu za kunakili (zinazotolewa katika miongozo ya walimu) na katika kupanga mpangilio ya darasani. | Mwalimu huwapa wanafunzi tatizo la "tiketi ya kuondoka" mwishoni mwa kila somo la hesabu, ambalo ni lazima walitatue kwa kutumia slaidi zao. Kwa kutumia kifuatiliaji, mwalimu anabainisha ni nani alikosea na anafikiria jinsi ya kuwasaidia katika somo linalofuata. Wanafunzi wakipata tatizo sahihi, mwalimu huacha kifuatiliaji wazi ili kupunguza mzigo wa kazi. | **Kutumia habari kulenga usaidizi**<br>**Vifaa:** Menyu ya shughuli za upimaji tamati ambazo walimu wanaweza kuchagua kutoka. Kifuatiliaji (kilichoandikwa au kielektroniki) cha kutambua umahiri wa wanafunzi wa umahiri muhimu wa KKK kwa wakati.<br>**Mafunzo:** Walimu huchagua mbinu za upimaji wanazotaka kufanya mtihani na kujifunza mbinu mbili hadi tatu ili kurahisisha matumizi yao ya taarifa za tathmini. (Kwa mfano *"Weka daftari zote za wanafunzi ambao walifanya vizuri sana kwenye kazi ya nyumbani ya hesabu katika rundo moja, na wale ambao walifanya vibaya kwenye rundo jingine. Siku inayofuata, vuta kitabu kimoja kutoka kwa kila rundo ili kuwaunganisha wanafunzi wawili."*)<br>**Usaidizi endelevu kwa walimu:** Wawezeshaji hufanya vipindi vya upangaji wa madaraja na kupanga na walimu ambapo huwauliza walimu kushiriki ni wangapi kati ya wanafunzi wao wako nyuma kwenye ujuzi au maudhui yanayofundishwa—na jinsi wanavyoweza kulenga usaidizi. wa hutumia video kujenga ujuzi wa walimu wa usimamizi wa darasa kwa shughuli za kikundi. |
| **Ngazi ya 3:** Kuanza mazoezi | Mwalimu anaandaa upimaji rahisi kutegemea na mawanda na mtiririko/lengo la kujifunza na kupanga makundi kulingana na maahitaji. Mwalimu anaingiza maswali yenye uwezo wa chini wa kufikiri, kisha anawauliza wanafunzi wafupishe na kufasiri maudhui waloyojifunza. | Wakati wa hatua ya kuandika kuhusu "kuandaa mazingira", mwalimu anaandaa orodha hakiki ya kupima aya ya mwanafunzi yenye maelezo kuhusu darasa lao. Mwalimu anawapa orodha hakiki yenye alama na iliyosahihishwa siku inayofuata. Wakati wanafunzi wanarejea aya waliyoandika, mwalimu anawachagua wanafunzi watano waliopata alama chache na kuwafundisha mmoja baada ya mwingine. Kwa wanafunzi watatu waliopata sifuri, mwalimu anawaambia wanafunzi waeleze kwa mdomo na kisha waandike majina ya vifaa wanavyoweza kuvibaini darasani. Baada ya hapo mwalimu anatoa usaidizi zaidi kwa wanafunzi hao wakati na baada ya klabu za skuli. | **Kujenga stadi za ngazi ya juu ya kufikiri**<br>**Vifaa:** Agiza maboksi au majalada yanayotoa fursa kwa ajili ya kuuliza maswali yanayowataka wanafunzi waeleze, watetee au kuthibitisha jibu lao. (Kwa mfano , *"wakadirie idadi ya punje za maharage kwenye jagi. Baada ya hapo waulize wanafunzi 2-3 waeleze namna walivyoweza kubashiri."*)<br>**Mafunzo:** Wawezeshaji wafafanue umuhimu wa mazingira chanya, salama na yenye kuhamasisha ambapo majibu ya kukisia na kutoa jibu lisilo sahihi yanapongezwa. Wawezeshaji wachanganye uzoefu wa mwalimu na ujifunzaji unaotokana na hisia za kijamii na mazingita( mazingira au mazingatio) ya muhtasari wa darasani.<br>**Usaidizi endelevu kwa walimu:** Washauri wa walimu waongoze mjadala pamoja na walimu namna ya kuwasaidia wanafunzi. Washauri waongoze majadiliano yenye tafakuri yenye kujielekeza kwenye maswali yafuatayo *"Katika andalio lako la somo, unadhani ni eneo gani ambalo wana- funzi wako wamelielewa vizuri? Ni eneo gani ambalo bado linawapa changamoto? Unajuaje? Unafanyaje kuhusu changamoto hizo. Walimu wachukue jukumu la uongozi unaokua wakati wa vipindi.*[23] |
| **Ngazi ya 4:** Mazoezi ya daraja la juu | Mwalimu anatengezeza shughuli tofauti za upimaji kutokana na mapitio ya muhtasari na vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji na kufanya maandalizi kutokana na mahitaji ya wanafunzi. Mwalimu akamilishe maswali ya ngazi ya juu ya kufikiri, awaulize wanafunzi kutabiri na kutathmini mawazo yao na mawazo ya wanafunzi wengine. | Kwa upande wa upimaji, mwalimu anamaliza siku kwa kuita wanafunzi tofauti tofauti kucheza mchezo wa ukadiriaji. Mwalimu anaandaa maswali kutoka kwenye daftari la mazoezi ya mwanafunzi kwa njia mazoezi ya wiki, mwallimu anawagawa wanafunzi wenye uwezo tofauti tofauti katika kila kikundi kupitia mradi wa mdomo ambapo kama kikundi wanakisia urefu wa vitu vitatu na kisha wanapima na kujadiliana kile walichokiona. Wakati wanafunzi wanafanya kazi zao, mwalimu anafuatilia na kuweka kumbukumbu katika maeneo ambayo yanawapa changamoto wanafunzi na kutumia matokeo hayo kupanga kipindi kitakachofuata. Wakati wanafunzi wanawasilisha, mwalmu anawauliza wathibitishe na kufanya tathi-mini ya makisio yao ya mwanzo na namba ambavyo makisio na vipimo vinaweza kutu-mika kwenye maisha yao ya kila siku. | **Kukuza upimaji binfasi na tafakari**<br>**Vifaa:** Ufuatiliji wa mwanafunzi, daftari la taarifa za kusoma na jarida la tafakuri, vifaa vya ziada vya utajirisho na ukabilisho<br>**Mafunzo:** Wawezeshaji wawasaidie walimu kujifunza na kufanya upimaji binafsi wa mwanafunzi na shughuli za upimaji rika<br>**Usaidizi endelevu kwa walimu:** Washauri wafanye kazi na walimu kubainissha shughuli za ukabilisho watakazo zitumia kwa wanafunzi wenye changamoto za kujifunza, kuwafuatilia na kujadiliana kuhusu kipindi cha ushauri kitakachofuata. Walimu wafanye mapitio na kujadiliana kazi za wanafunzi au kujirekodi video wakati wanafundisha, baada ya hapo wanaangalia video kwa kuonyesha maeneo wanayofanya vizuri na muda ambao wanafunzi walionyesha kuchanganyikiwa. |

Kama ilivyooneshwa hapo juu, moja ya changamoto ya msingi ambayo walimu wa ngazi ya 1 na 2 juu ya matumizi yao ya upimaji-Wanayoweza kukabiliana nayo ni kujua nini wapime na wakati gani. Changamoto nyengine mbili za msingi ni uwekaji wa kumbukumbu na kufuatilia matokeo (muda unaotumika) na pengine ni muhimu sana kwenye Upimaji kwa ajili ya kujifunza ni kujua namna ya kutumia matokeo. Upimaji unapokuwa mahali sahihi kulingana na madhumuni, mbinu mbali mbali za upimaji endelevu zikijumuisha zilizoorodheshwa kwenye jedwali la 3, zinaweza kuwasaidia walimu kuogelea kwenye upimaji kabla, wakati na baada ya kufundisha. Msingi wa utekelezaji wenye mafanikio hutokea pale mbinu ilyochaguliwa huleta maana kwa walimu, na kuonekana zina thamani na wanafurahia kutumia taarifa zinazotokana na upimaji. Wakati wa kuchagua au kutengeneza vifaa vya upimaji endelevu kwa ajili ya programu ya KKK, urahisi wa kutumia vifaa hivyo ni jambo muhimu. Tumia jedwali hili kubaini utendaji wa upimaji rahisi ambao unaweza kuongezwa kama njia ya kuleta mafanikio ya haraka katika programu ya KKK au kujumuishwa wakati wa kuandaa afua inayofuata

.**Jedwali la 3. Illustrative assessment techniques for instructional decision-making**


| | KABLA YA KUFUNDISHA<br>NI NINI? KIFAA HIKI KINA MAANA GANI? (HIKI NDICHO NINA-CHOTAKA KUPIMA?) | WAKATI WA KUFUNDISHA<br>ITACHUKUA MUDA GANI? NITAWEZAJE KUFUATILIA UJIFUNZAJI WA WANAFUNZI? | BAADA YA KUFUNDISHA<br>NAWEZAJE KUBADILI MPANGO KUTOKANA NA MATOKEO HAYA? |
|---|---|---|---|
| **Kidole gumba juu/ Kidole gumba chini, taa za kuongozea magari, tabasamu/uso wa huzuni** | Wanafunzi wanaonesha uelewa wao au wanajibu ndio/ hapana/kujibu maswali ya kweli/sikweli kwa kutumia sehemu ya mwili kama kidole gumba, mikono au kwa kujieleza | *Muda kidogo*<br>Kwa haraka chunguza mwitikio wa wanafunzi. | Kama umepata mwitikio hasi kama vile kidole gumba chini/uso wa huzuni kwa theluthi moja ya wanafunzi ifundishe dhana hiyo tena kabla ya kuendelea mbele. |
| **Kanuni ya kutonyanyua mkono** | Mwalimu anawaita wanafunzi bila kufuata utaratibu badala ya wanafunzi kuinua mikono wakati wa kujibu swali. Mbinu hii inaongeza "tija" kwa wanafunzi kwa sababu huwafanya wanafunzi wawe makini zaidi na kuwa tayari kuitwa. Mbinu hii humpa nafasi mwalimu kuwachagua wanafunzi wenye aibu na wale wa- siopenda kujibu maswali.<br>Angalizo: Shughuli hii inaweza kuwa ya kutisha kwa baadhi ya wanafunzi na inapaswa kutanguliwa na mijadala ya washirika au shiriki fikira.. | *Muda kidogo*<br>Waite wanafunzi waliokaa nyuma ambao hawajajibu swali kwa muda mrefu. Japo njia hii inatumia muda vizuri ila inahitaji uwepo wa mazin-gira salama na wezeshi ya darasa. | Angalizo katika kufuatilia, mwanafunzi ambaye hakuweza kujibu swali au aliyekosa swali unatakiwa kukutana naye baada ya kipindi ili kujua uelewa wake na hisia zake kuhusu shughuli ya kujifunza iliyofanyika darasani. |
| **Tiketi ya Kutoka** | Kila mwanafunzi lazima amalize kazi dakika 3-5 kabla ya kuondoka kwenye somo au kutoka darasani.<br>Kkazi hii inawezakufanywa kwenye kipande cha ubao au karatasi au kwa mdomo. Mbinu hii humsaidia mwalimu kuelewa ufahamu wa kila mwanafunzi kuhusu sehemu ya umaudhui ya somo husika. | *Muda wa Wastani*<br>Pitia kwa haraka tiketi za ku- toka mwisho wa kipindi, wakati wa kazi huru au wakati wa mapumziko. | Unda jozi kwa kuzingatia wanafunzi waliopata tiketi za kutokea na wale waliokosa. Kama idadi ya wanafunzi waliokosa tiketi ya kutokea ni wengi, rudia kufundisha mada hiyo. Na kama idadi ya wanafunzi waliokosa ni ki-dogo, panga muda wa ziada wa kutoa msaada zaidi. |
| **Jaribio la wiki** | Kifaa hiki hutoa taarifa kuhusu umahiri wa mwanafunzi audhui aliyojifunza kwa kutumia utaratibu unaojirudia 5 hadi 10 ya wazi na yaliyofungwa) kwa kutumia vifaa vilivy-mazoezi na vitendo vya wiki iliyopita. | *Muda kidogo*<br>Sahihisha majibu ya wana-funzi, weka kumbukumbu kisha warejeshee wanafunzi na wazazi. | Bainisha na sherehekea maudhui na stadi ambazo wanafunzi wamejenga umahiri. Bainisha na kufanya marudio ya maudhui na stadi ambazo zina akisi maswali ambayo wanafunzi wangi wamekosa. Weka mkazo au marudio zaidi kwa wanafunzi ambao hawaku-fanya vizuri kwa ujumla. |
| **Jarida la taarifa** | Wanafunzi hutumia jarida la taarrifa kufafanua uelewa wao, kuttoa maelezo, na waonnyeshe ujuzi wa kuandika. Hii inawezesha mwalimu apate maarifa ya kina katika uelewa wa wanafunzi, ujuzi wa mawasiliano ya maandishi, na, wakati mwingine, hisia zao au ustawi. | *Muda kidogo*<br>Soma kila alichojaza mwanafunzi , kisha weka kumbukumbu za alama ali-zopata. | Waweke wanafunzi katika makundi kulingana na namna walivyoonyesha uelewa wao katika mada husika au katika stadi ya kuandika. Kwa wana-funzi wanaopata shida ya kuandika, wachunguze kwa undani ili kujua uelewa wao dhana husika kwa njia ya mdomo ili ujue ni mahali gani wanapo-hitaji msaada wa ziada katika stadi ya kuandika. |

| | KABLA YA KUFUNDISHA<br>NI NINI? KIFAA HIKI KINA MAANA GANI? (HIKI NDICHO NINA-CHOTAKA KUPIMA?) | WAKATI WA KUFUNDISHA<br>ITACHUKUA MUDA GANI? NITAWEZAJE KUFUATILIA UJIFUNZAJI WA WANAFUNZI? | BAADA YA KUFUNDISHA<br>NAWEZAJE KUBADILI MPANGO KUTOKANA NA MATOKEO HAYA? |
|---|---|---|---|
| **Maswali** | Mwalimu anauliza maswali ambayo yanawataka wanafunzi kufikiri. Kifaa hiki kinamwezesha mwalimu kutathmini uelewa akati huo huo wakijenga fikra tunduizi and stadi ya kufikiri. | *Muda wa wastani*<br>Wakati wa kipindi, orodhesha majina ya wanafunzi wanaoshindwa kujibu maswali, kisha weka alama ya nyota kwenye swali linalo-fuata ambalo wanafunzi wachache walijaribu kujibu wa walijibu kwa usahihi. | Fanya mapitio ya maswali ambayo yamekuwa ni changamoto kwa wana-funzi. Angalia (kwa mwanafunzi mmoja mmoja au kwa vikundi vidogo vidogo) kwa wanafunzi walioandika jibu lisilo sahihi. |
| **Kuandika orodha hakiki** | Mwalimu awape wanafunzi maeneo 3 hadi 5 yanayokusudiwa na tathmini kuongoza uandishi wao au na washirika wao (Kwa mfani kichwa cha habari, uwekaji wa alama za uandishi; msamiati). | *Muda wa wastani*<br>Waache wanafunzi wajipime wao kwa wao; mwalimu atathmini mfano wa uandishi wa mwanafunzi. | Katika eneo la kuandika, baisnisha eneo ambalo utalirejea katika vipindi vitakavyofuata. |
| **Mfumo wa uwasilishaji wa wana-funzi** | Kwa njia ya mdomo, kuona au uwasilishaji kwa njia ya sanaa ambao umepata maksi kwa kupitia vigezo tofauti ambayo vimewasilishwa kabla. Kifaa hiki humsaidia mwalimu kupima ufahamu kwa wanafunzi kutumia njia nyingine zaidi ya majaribio na kazi za kuandika. Inawapa wanafunzi muda wa kujiandaa na vizuri kuwajulisha mapema maeneo ambayo watafanyiwa tahmini. | *Muda kidogo*<br>Sahihisha katika muda halisi, na baadaye weka kum-bukumbu za maksi. | Jiridhishe kama wanafunzi wame-jenga umahiri wa kutosha kwenye maudhui husika au unahitajika muda wa ziada wa kufundisha eneo maalum. |
| **Mazoezi ya washirika** | Waruhusu wanafunzi kufikiri kuhusu washirika wao (na baadaye wao wenyewe) mchakato wa kujifunza wakati huo huo mwalimu anachunguza. Inawasaidia wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kupokea mrejesho. | *Muda wa wastani (maandalizi)*<br>Andaa kiolezo au vigezo rahisi ambavyo wanafunzi watavitumia kupeana mre-jesho wao kwa wao. Chun-guza jozi wakati wanafanya kazi, waambie wanafunzi ku- toa taarifa na kuweka kumbukumbu za maksi. | Jaribu muungano tofauti wa wana-funzi (Kwa mfano kama wanafunzi wawili wana changamoto, waweke katika jozi na wanafunzi wawili ambao wameonyesha kujenga umahiri husika). |
| **Kuhesabu namba kwa pamoja** | Wanafunzi wamegawanywa katika vikundi 4, Walimu wanawasilisha swali na kikomo cha muda. Wanafunzi wanafanya kazi kwa pamoja kutafuta jibu la swali husika, baada ya hapo mwalimu anaita namba (1 hadi 4). Kikundi chenye namba hiyo kinajibu swali husika<br>Zana hii inawapa wanafunzi fursa ya kuuliza maswali ya kufuatilia na kuhalalisha majibu yao. Mwalimu ana uwezo wa kuangalia uelewa wa sampuli ya wanafunzi huku wanafunzi wote wakihakiki kikamilifu. | *Muda kidogo*<br>Ongeza muda wa kupitia makundi yote kujua namna walivyopata majibu.<br>Angalia wanafunzi ambao hawakuweza kueleza namna walivyopata majibu ya maswali, makundi ambayo yamepata majibu yasiyo sahihi zaidi ya moja, na maswali am- byao yalikuwa magumu ku- jibiwa.<br>Unapotumia mbinu hii mara kwa mara, huwafanywa wanafunzi wazoee kuunda makundi kwa kuhesabu namba. | Fanya mapitio ya dhana ngumu mara moja au wakati wa kuanza kipindi siku inayofuata. Toa msaada wa zi- ada kwa wanafunzi wanaopata changamoto ya kujifunza wakati wa kazi za kujitegemea. |

Matumizi yanayofaa ya upimaji endelevu hasa kwa walimu wanaoso- gea kwenye daraja la 3 na 4 hutegemea na hali ya darasa, utamaduni na uwezo wa mwalimu kusimamia darasa. Walimu ambao wameanzisha utaratibu wa kuwaweka wanafunzi katika makundi na kuwafanya watulie kila wanapofikia mwisho wa kipindi watakuwa wenye faraja zaidi kutumia na kutekeleza upimaji endelevu. Wanafunzi wanaopenda kujaribu hata kama hawapati jibu sahihi na wale wanaopewa fursa ya kuchagua na kuzungumza kwa

**MBINU PENDWA YA MWALIMU DEE**

Mwalimu Dee anapenda kutengeneza makundi kwa kuhesabu namba (Angai jedwali la 3).



Wakati wa mafunzo katika ngazi ya wilaya, mwezeshaji aliwaambia walimu wajibu maswali ya wazi kwa namna hii. Ilikuwa ni mbinu ya kufurahisha, Mwalimu Dee aliona namna mbinu hii inaweza kumsaidia kujua ni kwa kiasi gani wanafunzi wake wameelewa maudhui na dhana. Alifanya marekebisho ya shughuli ya upimaji kwa wanafunzi 60 kwa ku- unda makundi yenye wanafunzi 5 ambao wali- fanya kazi kwa pamoja kupata jawabu la ku- jumlisha swali lenye tarakimu mbili. Mwalimu Dee alichagua kikundi kimoja kuchunguza wakati makundi mengine yakijibu maswali sita ya kuhesabu. Wanafunzi walipenda shughuli hii kwa sababu walijua kuwa kuna muda utafika watatakiwa kuwasilisha kazi waliyofanya, kwa hiyo walifanya kazi kwa juhudi ili wajue kujibu maswali waliyopewa. Alipowaita namba 2 kutoa jibu la swali la 1, kwa mfano aliwauliza wanafunzi kutoka kwenye makundi mawili kuonesha namna walivyopata majibu. Mbinu hii ilitoa fursa ya kufanya mapitio na kumpa Mwalimu Dee uelewa wa kina kuwa ni hatua zipi zimeonekana kuwa ngumu kwa wanafunzi.

uhuru watakuwa na mwitikio chanya kwenye upimaji endelevu. Kwa mfano kama mwanafunzi anaadhibiwa kwa kutoa jibu lisilo sahihi atakuwa mwoga kujibu maswali wazi, swali la ngazi ya juu ya kufikiri. Kinyume chake, kama mwanafunzi akipongezwa kwa kujitolea akiwa darasani, itawa- jengea kujiamini kutetea au kufafanua mawazo yake bila woga. Kwa kuwa mazingira mazuri na usimamizi endelevu wa darasa ni chang- amoto katika darasa lenye wanafunzi wengi, lugha mchanganyiko, darasa lenye wanafunzi wenye changamoto mbalimbali za kujifunza na madarasa ambayo yapo kwenye maeneo yenye mgogoro, mbinu za upimaji zinatakiwa kurekebishwa ili zikidhi mahitaji ya muktadha. Watu sahihi wanaotakiwa kuzijaribu na kuzifanyia marekebisho mbinu husika katika programu ya KKK ni walimu wenyewe kwa kupata msaada wa kutosha.

**DOKEZO KUHUSU ISTILAHI**

Istilahi zinazohusiana na tathmini hutofautiana katika nchi mbalimbali. Neno "tathmini endelevu" linatoa mfano mzuri wa hii. Kwa maana ya jumla, "tathmini endelevu" inarejelea tathmini zozote zinazoendelea ambazo walimu hutumia kama sehemu ya mafundisho ya kila siku. Nchi nyingi, hata hivyo, zimetumia neno hilo katika uanzishaji wa "Mifumo ya Tathmini Endelevu" ambayo inajitahidi kuondokana na mitihani ya juu kwa ajili ya kuamua kupandishwa kwa wanafunzi. Kwa bahati mbaya, hii "Mifumo ya Tathmini Endelevu" mara nyingi imebadilika na kuwa mifumo changamano ambayo walimu wanaona ni ngumu kuelewa, ngumu na inayochukua muda kutekeleza, na inayolenga kugawa alama badala ya kuarifu maagizo. Neno "tathmini endelevu," kwa hivyo, lazima litumike kwa uangalifu katika muktadha wa kubuni mbinu za upimaji darasani; na katika nchi ambapo tathmini endelevu inahusisha kazi ngumu kwa walimu, unapaswa kuzingatia kutumia neno tofauti ili walimu wasihusishe kazi na kazi ngumu kupita kiasi na zisizo halisi.

## Mwalimu anawezaje kusaidiwa kupima ujifunzaji kwa wanafunzi wengi?

Utafiti wa hivi karibuni wa Julius Atuhurra na Michelle Kaffenberger umechunguza mtaala na mfumo wa mitihani kwa nchi ya Uganda na Tanzania kwa kutumia Utafiti wa Mbinu za Mtaala uliopitishwa kwa masomo ya Kingereza na Hisabati. Waandishi wa utafiti huo wamegundua kutoshikamana kwa hali ya juu kati ya mitihani ya kitaifa na viwango vya mtaala kwa nchi zote mbili. Kwa mfano kwa nchi ya Uganda ni mada 4 kati ya 14 katika viwango vya mtaala wa Kiingereza zilipimwa katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi. Wakati mada 2 ambazo zilionekana kuwa ni za kiupaumbele katika mtaala hazikuwemo kwenye mtihani. Kuhusianisha mtihani rasmi, ufundishaji na mtaala ni muhimu katika kutoa motisha ya ufundishaji wenye ubora wa kiwango cha juu.[24]

Kwa sababu walimu wengi wanaotekeleza programu ya msingi wa kusoma na kuandika hawana ufahamu mpana wa utekelezaji wa upimaji kwa ajili ya kujifunza, sehemu hii itaangazia ni kwa namna gani afua zenye kutekelezwa kwenye maeneo makubwa inaweza kufungamanishwa na msaada kwa walimu wa daraja la 1 na 2.

### KUIMARISHA UELEWA WA MUKTADHA


Kuna sababu nyingi za kimazingira ambazo zinaweza kuongeza wepesi kwa mwalimu kuziunganisha na upimaji kwa ajili ya kujifunza katika ufundishaji. Ni muhimu kubainisha sababu hizi na kuzitumia vizuri.

**Sera ya Upimaji:** Nchi nyingi zina sera ya upimaji, lakini nchi hizi zi- naweza au zisiweze kujumuisha upimaji darasani kwa uwazi, na mara nyingi haziimarishi upimaji kwa ajili ya kujifunza Chunguza sera zinazo shawishi upimaji wa darasani wa sasa na kuan- galia kama upimaji huo upo kwa mujibu wa bodi ya taifa au bodi ndogo ndogo na kuchunguza kama zinahusiana na kanuni za upimaji kwa ajili ya kujifunza na mitaala. Mara nyingi, hulenga upimaji usio rasmi. upimaji endelevu unaweza kumsaidia mwalimu kupata taarifa muhimu juu ya ufundishaji wao hata kama kuna fursa chache za kubadilisha upimaji rasmi unaotumika.

**Mshikamano wa mfumo:** Angalia kama kuna uhusiano kati ya upimaji katika ngazi tafauti na malengo ya mtaala. Kuna ushahidi mkubwa wa kutokuwiana sana kati ya mtaala, ufundishaji naupimaji (Angalia kwenye kisanduku). Kutokuwiana huko kunawapa walimu changamoto ya kutokujua kitu gani wakipe kipaumbele katika upimaji wa darasani na namna ya kutumia matokeo ya upimaji.

Pale ambapo taarifa za upimaji endelevu au tamati zinapatikana kwa urahisi, angalia mapungufu yaliopo katika ngazi za mikoa baina ya kile kinachopimwa na namna ambayo wanafunzi wanafaulu katika upimaji huu. Hii itakuwa taarifa muhimu wakati wa kuandaa mikabala ambayo itawagusa wanafunzi pale ambapo patakuwa na upimaji kwa ajili ya ujifunzaji uliokuwa mzuri na hatimae itawasaidia kufikia malengo yao ya ujifunzaji.

**WANAFUNZI WA MWALIMU DEE WANAOZUNGUMZA LUGHA NYINGI**



Mwallimu Dee anafurahia kuwa wanafunzi wake wanatoka sehemu tafauti za nchi na wanazungumza lugha tafauti – hali hii inafanya upimaji wa ujifunzaji kuwa mgumu. Kwa mfano, hivi karibuni alitoa zoezi la fumbo (katika lugha ya kujifunzia na kufundishia) darasani. Wanafunzi wote wanaozungumza lugha ya watu

wachache ( wakiwemo wanafunzi mahiri wa somo la Hisabuati) walishindwa kujibu hilo swali. Matokeo hayo yalimfadhaisha Mwalimu Dee na wanafunzi wake. Katika kuoanisha na vifaa vya programuu, programu ilibuni benki yenye kipengele cha upimaji katika lugha tafauti kikiwa na majibu. Baada ya hapo Mwalimu Dee alitumia kipengele hicho katika kupima wanafunzi katika somo lake bila kutumia nguvu za ziada. Pia aligundua ni kwa namna gani wanafunzi wake wenye kuzungumza lugha nyingi walivyokuwa na shauku ya kufanya zoezi alilowapa!

Programuu ya KKK yenye ufanisi itawahimiza walimu kutumia upimaji rahisi ambao unahusianisha na mbinu za ufundishaji pia muundo kwa ajili ya kuwakuza waanafunzi, usimamizi wa walimu na tathmini. Ukifanya kazi na mfumo uliopo unaozunguka upimaji wa darasani utaifanya programu yako kuwa imara; tazama *Ufundishaji – Unaozingatia Matokeo ya Upimaji: mwongozo wa hatua za mifumo* kwa ajili ya mjadala kuhusu namna ya kushughulika

kutokushikamana katika ngazi ya mifumo.

**Kipi kinatokea darasani:** Ni muhimu sana kuelewa namna sera ya upimaji inavyotekelezwa, kwa kuwa imani na utendaji wa sasa wa walimu, walimu wakuu na maafisa wa elimu ngazi ya serikali za mitaa utakuwa na ushawishi wenye nguvu kuhusu utayari wao wa kutekeleza Upimaji kwa Ajili ya ujifunzaji. Vile vile ni muhimu kujua ni ngazi gani ambayo walimu wanaanza nayo kwa ujumla ili kuweza kukadiria ni kiasi gani cha msaada wanachohitaji.

Tembelea ofisi za serikali ngazi ya seriakli za mitaa na walimu wakuu kuona kama ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji umepewa thamani inayostahki. Omba uweze kuona mitihani iliyopita ya kupandishwa daraja , kadi za ripoti au ushahidi wowote unaonesha kuwa upimaji umejumuishwa kwenye kupandishwa wanafunzi. Jadili uzito wa nyaraka hizo katika kufanya maamuzi kuhusu ufundishaji wa walimu na kiwango ambacho hata upimaji wa kiwango cha chini kwa mfano jaribio la mwezi, na mazoezi ya kila wiki yanatumika kutengeneza tathmini kubwa. Aina hii ya uainishaji inatakiwa ifanyike kwa kufikiri kwa kina, kwanza kwa kupitia ripori na tafiti zilizopo, na pia kupanga kutembelea skuli chini ya uratibu wa taasisi za serikali na washirika wanaofanya kazi zinazofanana na hizi. Taarifa za pamoja kuhusu ukubwa wa darasa, kiwango cha kurudia darasa, lugha ya kwanza ya kujifunzia, ukatili wa kijinsia katika ngazi ya skuli na kuenea kwa ulemavu unaweza kuwa ni muhimu kwa ajili ya kujenga nadharia kuhusu vikwazo vya kuanzisha ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji. Pia ni muhimu kubaini rasilimali, uzoefu, mitazamo na lengo la pamoja linaloweza kuwekwa ili kuleta Upimaji kwa ajili ya ujifunzaji. Mahojiano pamoja na walimu yanaweza kuthibitisha au kuongeza vikwazo na rasilimali, ushirikishwaji wa walimu katika kila hatua ya kubuni na kujaribu mchakato utasaidia kufanya mbinu na mchakato unaowafundisha walimu kuwa wa maana na unaotekelezeka.

> Akyeampong et al. walifanya utafiti kuchunguza hali ya sasa ya ufundishaji wa walimu na utendaji wa upimaji na kubaini athari za mafunzo ya walimu kazini. Mwandishi alikusudia kuona hali ilivyoenea katika nchi za Afrika zilizo katika ukanda wa jangwa la Sahara. Mara nyingi walimu wameonekana kama wenye kutoa mamlaka na wanafunzi wanatarajiwa kuwa wasikivu na kukariri majibu pasipo kuwa na upimaji kwa ajili ya kujifunza. Kwa kuongezea, uelewa wa walimu kuhusu upimaji unalenga wanafunzi kukumbuka ukweli waliokariri. Kubadilisha mazoea haya yaliyozoeleka yanatakiwa yaende taratibu ya kilenga kiwango cha juu chenye kuleta mabadiliko rahisi.[26]

> kifaa cha benki ya dunia cha kuangalia ufundishaji wa mwalimu kinajumuisha vigezo vya kukusanya taarifa kuhusu ufanisi ambao walimu hutumia kupima uelewa, kutoa mrejesho na kukuza fikra tunduzi kupitia maswali yaliyowazi.[25]


Uchunguzi wa darasani kwa jili ya kuchunguza ngazi ambayo walimu wanaanza nayo unatakiwa kuzingatia yafuatayo:


- Matumizi ya walimu ya upimaji rasmi na usio rasmi
- Matumizi ya walimu ya ngazi tafauti za kuuliza maswali (Kufupisha, kutafasiri, kutabiri, kutathmini)
- Mwitiko wa walimu kwenye majibu ya wanafunzi yaliyo sahihi na yasiyo sahihi.
- Kumbukumbu za walimu kuhusu upimaji wa aina yoyote.
- Mwalimu anafanya kwa vitendo uundaji wa makundi, kutafautisha ufundishaji kutokana na mahitaji au kuongeza umakini kwa mtu mmoja mmoja kutokana na matokeo ya upimaji
- Mwalimu anabadilisha kasi, mbinu au kurudia kufundisha somo kutokana na matokeo ya upimaji

Uchunguzi huu unapaswa kufuatiwa na mahojiano na walimu ambayo yanauliza maswali manne muhimu kwa walimu kuzingatia (yaliyoainishwa hapo juu katika "Ni kwa namna gani walimu wanapima kwa ajili ya ujifunzaji?") na ambayo pia huuliza juu ya ujuzi wao wa upimaji wa darasani (Je! , unaweza kuielezea?) na mtazamo wao kuhusu tathmini darasani kwa ujumla. Hata ziara chache za shule katika wilaya nyingi zinaweza kukusaidia kuamua ni daraja gani walimu wako wengi wako kwenye kuhusiana na tathmini ya uundaji, na, kwa upande wake, jinsi ya kufanya.
wasaidie kusonga mbele. Wakati wa kuwasilisha matokeo haya, ni muhimu kwanza kufafanua tofauti kati ya muda uliotengwa kwa ajili ya tathmini ya uundaji dhidi ya muhtasari, na kuonyesha tofauti kati ya tathmini ya uundaji na urudiaji wa mwanafunzi (simu na majibu). Wadau wanapochanganya haya, wanaweza kuamini kuwa maagizo ya ujifunzaji yanatokea zaidi kuliko yalivyo.

**KIELELEZO 4.**
**Kazi za upimaji darasani zimejumuishwa kwenye vifaa vya Funda Wande**

## Wiki 3: Siku 5




### Sauti za herufi (Foniki) Upimaji (dkk 15)

**Vifaa**:Kadi zenye herufi ya sauti zilizofundishwa; kadi zenye maneno yenye sauti /p/ na /r/

**Maandalizi**: Hakikisha kila mwanafunzi ana kadi za sauti zote walizofundishwa. Hakikisha kuna kadi mbili, kadi moja yenye neno linaloanza na /p/ na kadi nyingine yenye neno linaloanza na /r/.

**Lengo la somo/masomo**: Bainisha na tamka herufi haraka. Soma maneno yenye herufi walizojifunza. Tunga sentensi fupi.

**SHUGHULI**

**1. Kadi za Herufi na sauti za herufi**

- Waambie wanafunzi kuweka kadi zao ziangalie kwa mbele ili waweze kuzisoma.
- Taja kila sauti ya herufi na kisha waambie wanafunzi kuchagua kadi ya herufi.
- Chunguza wanafunzi wanaopata ugumu kuoanisha sauti na herufi.

**2. 2. Maneno ya sauti za herufi**

- Mpe kila mwanafunzi kadi, hakikisha kila neno lipo kwenye kadi nyingine.
- Waambie wanafunzi kuwa utataja neno husika na wanafunzi wawili wenye neno ulilotaja watasimama na kubadilishana mahali pa kukaa.
- Kwa kila neno:
  - Sema = itoti.
  - Tenganisha katika sauti = i/t/o/t/i.
  - Unganisha sauti kuunda neno = itoti.
  - Rudia kama ni lazima kuhakikisha wanafunzi wanapata uzoefu wa kutosha.
- Wape nafasi wanafunzi wote kusoma na kubadilishana mahali pa kukaa.

# Mtaala na Vifaa

Kuhusu maeneo mengine ya kufundisha KKK, mwongozo wa mwalimu unaweza kutumika kama kifaa cha usaidizi kum- saidia mwalimu kutumia ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji. Upimaji kwa ajili ya ujifunzaji unatakiwa uin- gizwe kwenye vifaa vya kufundishia kila wakati. Ni kweli kuwa walimu wa ngazi ya 4 wanaweza kutumia mtaala kuen- deleza, kutumia na kuchanganua mbinu zao wenyewe za upimaji. Walimu walio kwenye ngazi ya 1 na 2 wanaweza kufaidika na mbinu rahisi za upimaji ambazo zimeingizwa kwenye mwongozo wa mwalimu. Kiwango cha maelezo ya wazi yaliyo kwenye mwongozo hutakiwa kuakisi kiwango cha walimu wengi walio katika muktadha husika. Hata hivyo walimu walio kwenye ngazi ya juu wanaweza

**KIELELEZO 5.** **Kilelezo cha mfano wa orodha hakiki ya upimaji**

| UTAMBUZI WA FONOLOJIA SHUGHULI ZA KUFANYWA NA MWANAFUNZI | JINA YA MWANAFUNZI | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Janet | Brenda | Abdul | Ishaan |
| Piga makofi sawa na idadi ya maneno katika sentensi rahisi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Piga makofi kwa maneno yaliy-ochanganywa | ✓ | ✓ | | ✓ |
| Tambua maneno yenye vina | ✓ | | | |
| Kwa mdomo tamka maneno yenye vina Baisinisha | | ✓ | | ✓ |
| maneno yenye vina | | | | ✓ |
| silabi kwenye maneno yenye silabi mbili au tatu | | ✓ | | ✓ |
| Unganisha na tenganisha kwa mdomo maneno yenye silabi tatu | | ✓ | | |

*Programuu inaweza kutengeneza kifaa cha kufuatilia (au kidigitali) kinachoweza kumsaidia mwalimu kuingiza jina la mwanafunzi na kuweza kujua umahiri wa mwanafunzi katika kipindi chote cha masomo.*


kufaidika kutokana na dokezo na vidokezo vilivyo kwenye mbinu za upi- maji. Mbinu zifuatazo kwa ajili ya kuunganisha mwongozi wa Upimaji kwa Ajili ya Ujifunzaji ndani ya vifaa vya ujifunzaji vinaweza kuwasaidia walimu kutumia ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji:

**Bainisha maeneo asili ya upimaji:** Jumuisha mfano wa upimaji da- rasani ambao unatoa mapende- kezo ya kutumia Upi- maji kwa Ajili ya Ujifunzaji kila siku na un- aopendekeza kulenga maeneo machache na kupendekeza muda wa kufanya upimaji endelevu na upimaji tamati ulio rasmi unaoen- dana na lengo la mtaala la kujif- unza. Baadhi ya vifaa vya ujifunzaji na ufundishaji kwa mfano mwon- gozo wa mwalimu umejumuisha mapendekezo rasmi kwa ajili ya upimani wa kila siku na kila wiki ambayo humsaidia mwalimu katika utekelezaji. Kwa mfano siku ya mwisho ya wiki inaweza kuoneshwa kama siku ya kufanya upimaji na mapitio ya siku, wakati walimu wanafanya upimaji endelevu wa maudhui ya wiki nz- ima na kufanya mapitio ya stadi ambazo zinawapa changamoto wanafunzi wengi au kutoa kazi endelevu kwa wana- funzi ambao wamemudu umahiri uliokusudiwa kwa wiki husika. Kwa walimu walio ngazi ya 3 na 4, ni muhimu sana kutoa msaada kwao kwa kutumia maswali ya kina–maswali ya wazi ambayo wanafunzi hawafikiri kama mwalimu anaweza kuwa na majibu.[27] Maswali yanayowataka wanafunzi kufafanua majibu yao ya mwanzo, au kuhusianisha na wazo jingine, kusaidia mabadiliko ya mchakato wa utambuzi wa wanafunzi na kuendeleza stadi za kiwango cha juu cha kufikiri. Swali la mfano linatakiwa lihusian-

**KIELELEZO CHA 6. Tangerine: Teach**

Tangerine: Teach husaidia Walimu kufahamu maendeleo ya mwanafunzi na umahiri wa kusoma na kuhesabu kupitia ukaguzi unaozingatia mtaala ulioimarishwa.

Kupitia upimaji wa haraka, walimu wanaweza kuonesha ni lini na wapi muda wa ufundishaji unatakiwa kuzingatia na kulinganisha na mwenendo wa utendaji dhidi ya alama teule na lengo. Ikiwa inafanya kazi bila mtandao, Tangerine: Teach hutoa taarifa ambayo ni rahisi kuitumia kumsaidia mwalimu kujua wanafunzi wake wanaofanya vizuri (wakionekana kwenye rangi ya kijani upande wa kulia), na wanafunzi wanaohitaji msaada kabilishi na uangalizi wa karibu (huonekana kwenye rangi nyekundu na chungwa.[28]



Ripoti iliyochaguliwa

Kupanga kwa Wanafunzi: Kitengo cha Barua 1

wanafunzi waliopimwa: 5 / 5

Wastani Sahihi 6 / 8 (75%)

Kupanga kwa Wanafunzi

| Mwana-funzi | alama | Asilimia | Hali |
|---|---|---|---|
| Erica | 8 / 8 | 100 % | Vyema |
| Dan | 7 / 8 | 88 % | Vyema |
| Carla | 6 / 8 | 75 % | Nzuri |
| Ben | 5 / 8 | 63 % | Nzuri |
| Anna | 4 / 8 | 50 % | Kawaida |


Maoni

40% - 59% Percentile

Wanafunzi hawa wanazidi kuwa bora.
Zingatia kutunga maoni yako
kwa wanafunzi hawa kama ifuatavyo:

Uliweza kusoma barua nyingi kwa usahihi na kwa kasi nzuri.
Hata hivyo unapaswa kuwa makini na chini yakobarua za kesi kama ulivyoandikamakosa machache zaidihapo.

**KIELELEZO 7. Mwongozo wa mwalimu unatoa mawazo namna ya kumsaidia mwana- funzi anayehitaji msaada wa ziada**



MAPITIO
Wiki 17 • Siku ya

Tusome
1. "Kasuku wa kijivu wa Kiafrika" Ukurasa 43
2. "Kwanini duma ana mashavu yenye madoa kama ma- chozi" ukurasa 47



*Let's Read* page 43

KUSOMA KWA UFASAHA NA UFAHAMU — 24 DKK.

Andika kichwa cha hadithi Tusome hadithi, idadi ya kurasa kama ilivyooneshwa upande wa kushoto

**# Sasa utasoma kitabu cha hadithi "Kasuku wa kijivu wa Kiafrika na"Kwanini duma ana mashavu yenye madoa kama machozi" kwa mara nyingine ukiwa na mwenzako jibu maswali hadi mwisho. Tafadhali rejea ukurasa wa 43 wa kitabu cha Tusome Kitabu.**

Je, wanafunzi wamejifunza wakiwa kwenye jozi? Kwanza, wachukue zamu ya kusomeana hadithi kwa sauti, wasaidiane kusoma kwa usahihi na kwa ufasaha. Kila mwanafunzi anatakiwa asome hadithi mara 2. Wakimaliza kusoma hadithi, washirika wanafanya kazi pamoja kujibu maswali ya ufa- hamu mwisho wa hadithi kwenye madaftari yao. Washirika wanapomaliza hadithi ya kwanza, wanaendelea kwenye hadithi ya pili

**Maelekezo Tofauti:** Shughuli hii ni ya wanafunzi ambao ni "Mkutano Matarajio." Unaweza kubadilisha shughuli hii kwa wanafunzi wengine katika njia zifuatazo:

- *Wanafunzi **Waliozidi Matarajio:*** A Mwanafunzi mwenye nguvu zaidi anaweza kuwa iliyooanishwa na mwanafunzi dhaifu ili kutumika kama mshauri rika na msaidie mwanafunzi kukamilisha shughuli. Vinginevyo, ikiwa wanafunzi wanatayari alijibu maswali ya ufahamu mapema katika kipindi,wana- weza kutumia muda huu kusoma wasomaji wa nyongeza au nyinginezo maandishi badala yake.
- *Wanafunzi Who **Wanaohitaji Usaidizi wa Ziada: Mwanafunzi dhaifu anaweza kuwa iliyoungan- ishwa na mwanafunzi mwenye nguvu zaidi kwa usaidizi wa kukamilisha shughuli.***

Tembea darasani na bila mpangilio chunguza kazi za wanafunzi, toa msaada pale unapohitajika.

ishe kitabu chenye kuendana na darasa husika na kuunganisha na maswali ambayo yanabeba dhana na kuuliza “kwanini”, “Kwa namna gani” kuliko kuuliza “Nini” na “Lini”. **Kielelezo 4** kinawasilisha mfano wa vifaa kutoka Afrika ya Kusini ambao unatoa mwongozo kwa walimu namna ya kutekeleza Upimaji kwa Ajili ya Ujifunzaji ndani ya darasa

**Fikiri athari za muda wa Upimaji:** Ikumbukwe kuwa Upimaji kwa Ajili ya Ujifunzaji usio rasmi hauhitaji muda wa ziada ila Upimaji kwa Ajili ya Kujifunza rasmi -– kuweka kumbukumbu za matokeo huhitaji muda wa ziada. Walimu ambao ni wageni kwenye kutumia Upimaji kwa Ajili ya Kujifunza rasmi wanaweza kuwa si wapya kwenye Upimaji kwa Ajili ya Ujifunzaji usio rasmi, kwa hiyo wanaweza kuona kuwa Upimaji ni mzigo na unahitaji muda wa ziada ambao wangeutumia kutekeleza mtaala. Kujumuisha Upimaji kwa Ajili ya Ujifunzaji kwenye vifaa inawasaida walimu kujifunza namna ya kutekeleza upimaji usio rasmi katika namna ambayo haichukui muda mrefu na vile vile kuhakikisha kuwa muda wa kutosha wa kutekeleza upimaji sahihi na kuweka kumbukumbu za matokeo unafanyika.

Mojawapo ya mbinu rahisi na zinazotumia muda mwingi katika ujifunzaji isiyo rasmi ni mwalimu kuzunguka darasani wakati wanafunzi wanafanya kazi na kuchunguza ujuzi wa mwanafunzi mmoja ,mmoja; Walimu wanaweza kukumbushwa kufanya hivi katika mwongozo wa mwalimu.

**Unda mfumo rahisi wa kutunza kumbukumbu za upimaji:** Mbinu rahisi za kuweka kumbukumbu za upimaji zinaweza kuunganishwa kwenye mwongozo wa mwalimu na kufundishwa kwenye mafunzo ya walimu kazini. Kwa mfano miraba fito yenye kazi za upimaji ikiwa ime- andikwa kando ya ukurasa na orodha ya majina ya wanafunzi upande wa juu inaweza kutumika kama ilivyoonyeshwa kwenye mfano uliopo kwenye **kilelezo cha 5**. Mfano unaweza kuonyeshwa kwenye mwongozo wa mwalimu pamoja na mbinu kwa ajili ya kuutumia.

Bila kujali ni orodha gani au chombo gani kinatumika, ni muhimu kusisitiza kuwa chombo hicho kimekusudiwa kuwasaidia walimu badala ya kuwafuatilia au kuwatathmini. Zana zozote zinazopaswa kutumiwa zinapaswa kuanzishwa wakati wa mafunzo, zikisaidiwa kupitia usaidizi unaoendelea wa walimu, na kuboreshwa kwa muda kulingana na maoni ya mwalimu. Waalimu hawapaswi kamwe kuadhibiwa kwa kutumia zana ya kurekodi “vibaya”—na, kwa hakika, kutumia zana kama hizo itakuwa hiari. Ikiwa walimu wanahisi kwamba chombo ni kizito au cha kutatanisha, huenda wakaacha kukitumia. Inapowezekana, teknolojia ni suluhisho zuri la kunasa data ya tathmini ya uundaji, kwani tathmini mpya zinaweza kuongezwa kwa urahisi kwenye kifuatiliaji kinachotegemea programu, kama vile mfano wa Programu ya ufundishaji wa Tangerine iliyoonyeshwa kwenye **kilelezo cha 6** Kiolesura safi kitazuia walimu kupata. kuchanganyikiwa au kulemewa, na algoriti zinaweza kuondoa kazi nyingi za uchanganuzi kwa walimu huku pia zikitoa maoni yanayoweza kutekelezeka.

**Jumuisha mikakati ya kutumia matokeo:** Mwongozo wa mwalimu pia unaweza kujumuisha vidokezo na mikakati ya kutumia matokeo ya KKK. Haya yanaweza kujumuisha vipindi vifupi vya mapitio, kazi za nyumbani zinazolengwa, vikundi vya baada ya shule, kupanga watoto katika vikundi kulingana na matokeo ya tathmini, na kuoanisha wanafunzi waliofanya vizuri na wa chini. Kuzingatia mambo rahisi ambayo walimu wanaweza kufanya kulingana na matokeo ya tathmini kunaweza kuwasaidia walimu kujisikia kuhamasishwa na kuwezeshwa kufanya tathmini ya darasani. **Kielelezo cha 7** kinaonyesha mfano wa mwongozo wa mwalimu kutoka Liberia ambao unatoa baadhi ya mapendekezo kwa walimu kuhusu jinsi ya kutofautisha maelekezo kulingana na matokeo ya tathmini.

# Maendeleo ya Kitaalamu  ya Walimu


## ELIMU YA UALIMU

Kozi za kufundisha kusoma na kuhesabu zinatakiwa kuunganisha upimaji wa maudhui ya darasani na kujumuisha vipengele vifuatavyo:

- Muktadha na urekebishaji wa mbinu mahsusi za Upimaji Kwa Ajili ya Kujifunza kwa muktadha wa mazingira ya darasa husika
- Kuhimiza mbinu za “Kufaa-Sahihi” (Wakati wa kutumia Upimaji endelevu dhidi ya Upimaji tamati)
- Kuonesha kwa mfano na vitendo maswali ya kiwango cha juu cha kufikiri

- Kuonesha kwa vitendo mbinu za kupima idadi kubwa ya wanafunzi
- Mbinu za Usimamizi wa darasa kusaidia uwezeshaji na matumizi ya upimaji
- Kuanzisha mazingira salama darasani na utamaduni unaolenga kuwasaidia wanafunzi kwa njia ya upimaji
- Mbinu za kuchukua, kutunza kumbukumbu na kufuatilia upimaji endelevu wa utendaji wa wanafunzi kwa njia rasmi na isiyo rasmi
- Uchanganuzi na kutafasiri matokeo ya upimaji kwa kuangalia nguvu za kipekee, uzoefu na mahitaji ya wanafunzi
- Uandaaji wa somo la kufundisha unaoshirikisha ushahidi wa upimaji endelevu
- Mbinu za kutumia matokeo kutoa mrejesho na kupanga urekebishaji  na uboreshaji
- Kuchunguza aina tafauti za upimaji na nafasi ya upimaji endelevu katika kuongeza matokeo ya upimaji tamati

**FURAHA YA MWALIMU DEE WAKATI WA MAFUNZO**




Mwalimu Dee alidhani kuwa siku 2 za mafunzo zilikuwa za kufurahisha. Mwezeshaji alianza kwa kuwauliza walimu waonyeshe mafunzo “kidole gumba juu” au “kidole gumba chini” kuonyesha mada ya hesabu wanaoipendelea. Mwalimu Dee hakuwahi kufahamu kuwa kila mtu hakuwa anapenda mada ya kugawa. Siku ya 2, mwalimu Dee na wenzake wakarekebisha mbinu ya “kidole gumba juu /kidole gumba chini” kuwa “simama juu/kaa chini” kama kichangamshi lakini kupima uelewa wa mada ya mafunzo iliyofundishwa wakati wa mafunzo. Zaidi ya yote, mwalimu Dee alijifunza kuwa michezo ya kufurahisha ni mbinu ambayo anaweza kuitumia wakati wa kufundisha darasani kwake.

## MAFUNZO YA WALIMU  KAZINI

Mafunzo ya kazini yanapaswa kujengwa juu ya yale ambayo walimu tayari wanayajua kuhusu tathmini na wanayoyafanya katika madarasa yao. Walimu hawahitaji tu kujifunza kuhusu tathmini lakini pia wanahitaji kufanya mazoezi ya kusimamia tathmini rahisi za kiutendaji na kutumia matokeo kutoa mrejesho kwa wanafunzi na kufanya maamuzi kuhusu mafundisho..

**TEACHER DEE’S MONTHLY COACH VISIT**



Today, the sector coach met with Teacher Dee for their monthly school visit- it was so encouraging! From their last phone call, she knew her coach would be observing for one thing: questioning. Teacher Dee prepared by writing the questions from the teachers guide on the board before the lesson started, and she remembered to also give students time to explain how they got their answer. Her coach was thrilled! After celebrating her good work, the coach asked her to think of one open-ended, higher order question she could ask about next week’s story. Her coach then shared with her a simple table for tracking students, and their responses and shared short videos of other teachers demonstrating examples of higher-order questioning.

Lengo la kwanza la mafunzo ya kazini—hasa kwa walimu katika daraja la 1 na 2—linapaswa kuzingatia kuhamasisha mabadiliko ya tabia iliyopangwa kwa kuonyesha jinsi mbinu mahususi za Upimaji kwa Ajili ya Kujifunza zinavyosaidia kuafikiwa kwa motisha zilizopo za walimu; kuweka hali ya udhibiti na ufanisi kwa walimu kupitia fursa za kufanya mazoezi na kutafakari mbinu za Upimaji kwa Ajili ya Kujifunza; na kuanzisha Upimaji kwa Ajili ya Kujifunza  vitendo kama kawaida miongoni mwa rika la walimu, mwanzoni kwa kuwaonyesha walimu hao ambao ni warekebishaji wa mapema. Mafunzo yanapaswa kuanza na majadiliano ya uzoefu wa awali wa walimu kwa kutumia matokeo ya upimaji katika kupanga somo. Ajenda ya mafunzo inapaswa pia kutoa muda wa kutosha wa kujadili na kufanya mazoezi ya ujuzi, mikakati, na shughuli zinazotumika wakati wa wa upimaji endelevu na upimaji tamati.

Lengo la pili la mafunzo ya walimu kazini ni kuhakikisha stadi na maudhui yanakuwa rahisi kueleweka na yenye malengo kadri inavyowezekana – kitu moja kwa wakati badala ya kufanya kila kitu kwa wakati mmoja. Pachika mbinu za upimaji zilizochaguliwa kutoka kwenye vifaa wakati wote wa mafunzo ili walimu wapate uzoefu huo mara moja. Mbinu nyingi za upimaji endelevu zinafurahisha kama zinawasilishwa kwa njia ya michezo. Upimaji endelevu ukifafanuliwa kwa uwazi, na ukatekelezeka kwa urahisi, na kuwasilishwa kwa njia ya michezo, kuna uwezekano mkubwa walimu wakau- tumia upimaji

endelevu darasani.

Lengo la tatu la mafunzo ya walimu kazini ni kuwapa walimu fursa ya kuwa na chaguo la kujifunza kwa vitendo upi- maji rahisi wakati wa mafunzo. Kufanya hivi kutawaaminisha kuwa mapendekezo tunayowapa wakati wa mafunzo kuhusu upimaji endelevu hayachukui muda mwingi kama inavyodhaniwa na kuwa ni rahisi. Hii inajumuisha kuwa na ch- aguo kwenye mbinu za upimaji: kwa mfano kuchagua kati ya chaguo mbili za kutumia michezo kwa walimu wa ngazi ya 1 na orodha ya mikabala kwa walimu wa ngazi ya 2 na 3. Kuunganisha mafunzo na jumuiya za kujifunza, mikutano ya walimu, na ziara za wanasihi elekezi kwa kuwataka walimu kujaribu mikabala zaidi wakiwa darasani na kutoa taarifa juu ya kilichojiri wakati wa ujaribishaji darasani na kipi wataweza kubadili kutokana na matokeo ya darasani.

## MSAADA ENDELEVU KWA WALIMU

Walimu wanahitaji msaada endelevu ili waweze kutekeleza kazi za Upimaji kwa Ajili ya ujifunzanzaji. Wanasihi elekezi wanatakiwa kujadili matokeo ya upimaji na walimu na kuwapa mwongozo namna ya kurekebisha ili kuakisi matokeo pale inapowezekana. Wanasihi elekezi waliomahiri zaidi wanaweza kuonesha mbinu rahisi zilizoungana na ngazi ya upimaji wa Ujifunzaji wa mwalimu wakiwa darasani; walimu wanapoona mbinu za Upimaji kwa Ajili ya ujifunzaji zinatumika katika madarasa yao, utekelezaji wake utafanikiwa. Wanasihi elekezi ambao hawana uelewa wa kutosha wa Upimaji kwa Ajili ya Ujifunzaji wanaweza kupewa video za mfano na walimu wengine kwa ajili ya kushirikishana na kujadiliana wakati wa ziara. Vifaa vya uchunguzi vya wanasihi elekezi, hasa vile vinavyotumika kwenye mfumo wa elimu vinatakiwa kuwa wazi na rahisi kuchunguza viashiria vya upimaji endelevu (kwa mfano, *"Je, wanafunzi walipewa fursa ya kujaribu au kutoa majibu yao wenyewe bila ya kushinikizwa na walimu? Mwalimu alijibu nini kwenye jibu sahihi na lisilo sahihi lililojibiwa na wanafunzi? Mwalimu alitulia na kusahihisha, au kurudia kufundisha wanafunzi walipoonesha kutokuelewa?"*).

Jumuiya za kujifunza (mahali pengine zinajulikana kama jumuiya za kitaalamu za kujifunza, mzunguko wa walimu wa kujifunza na istilahi nyengine kutegemeana na nchi) inaweza kuwa ni mahali kwa walimu kushirikishana uzoefu katika kutumia na kurekebisha upimaji endelevu na kujadiliana namna watakavyotumia taarifa katika kupanga somo la siku au wiki inayofuata. Kwa mfano, walimu wanaweza kuchagua mbinu moja ya upimaji endelevu kutoka kwenye chaguo la orodha katika kipindi kimoja, wakaijaribu mbinu hiyo darasani na kushirikishana vidokezo baadaye. Jumuiya za Kujifunza na mikutano ya walimu ni fursa nyingine kubwa kwenye utengenezaji wa zana, kusahihisha upimaji/uchanganuzi na andalio la somo. Hii huwafanya walimu waone kuwa muda wao haujapotea na kuruhusu maswali ambayo huwasaidia walimu kubaini na kuziba mapengo wakati wa ujifunzaji wa wanafunzi

> Mradi wa Kusoma wa TA nchini Ethiopia uliofadhiliwa na USAID uliandaa moduli iliyolenga upimaji wa darasani katika skuli za msingi, ulijumuisha uundaji wa makundi na namna ya kutafautisha ufundishaji kwa kuzingatia mahitaji tafauti ya kujifunza ya wanafunzi.
>
> Moduli ilijumuisha mbinu za upimaji rasmi na usio rasmi katika maeneo matano ya ku- soma (Ufahamu wa fonemiki, grafonemiki, msamiati, ufasaha na ufahamu) pamoja na kuandika. Kazi zilijumuisha uchanganuzi wa kisa mafunzo za kujifunza ubainishaji wa mahitaji ya kujifunza. Wakati wa mahojiano ya vikundi maalum vya wakufunzi na walimu, wahojiwa walisema mbinu za upimaji zilikuwa sahihi kwa muktadha na zenye maana kwa sababu zilijumuishwa katika madarasa ya kusoma.

# Hitimisho

Programuu za KKK zinalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajenga umahiri kwenye stadi za kusoma na kuhesabu ili waweze kufanikiwa skuli. Ni muhimu sana kwa walimu kufuatilia maendeleo ya wanafunzi na kutoa msaada unaohitajika kuwasaidia wanafunzi kujenga stadi husika. Kwa kutambua mwendelezo wa ufahamu na stadi ambazo mwalimu anazo katika kutekeleza ufundishaji unaozingatia matokeo ya upimaji, msaada na mwongozo kwa walimu unatakiwa ulenge kuwawezesha walimu kujumuisha mbinu za upimaji katika ufundishaji. Walimu wakiwa na uwezo wa kutafakari kama wanafunzi wamejifunza stadi na maudhui yaliyotarajiwa, na kuchukua hatua stahiki kama wanafunzi hawakujifunza stadi na maudhui yaliyokusudiwa, walimu watakuwa kwenye ufanisi zaidi katika kuimarisha matokeo ya ujifunzaji kwa wanafunzi wote darasani.

## MAREJELEO

**Go-to resource when mapping the assessment context where your FLN program is working:**
**https://riseprogramme.org/publications/aligning-levels-instruction-goals-and-needs-students-aligns-varied-approaches-common**

## UTAALAMU UNAOHITAJIKA

- Maagizo ya kusoma au hisabati, kwa kuzingatia maalum juu ya tathmini ya uundaji, kusaidia maendeleo ya modeli ya tathmini ya darasani.
- Maendeleo ya kitaaluma ya walimu (kabla ya huduma, mafunzo ya ualimu, na usaidizi unaoendelea wa walimu) ili kusaidia ujumuishaji wa tathmini ya darasani katika mifumo ya maendeleo ya taaluma ya walimu.
- Usimamizi wa darasa na hali ya hewa ya shule, kubuni mikakati inayoitikia kimuktadha kwa ajili ya kuwezesha aina mbalimbali za tathmini na kwa ajili ya kulenga na kurekebisha wanafunzi wanaotatizika.
- Uchanganuzi wa data ya kimsingi na mawasiliano, ili kutengeneza umbizo na kiolezo cha walimu ambacho hufanya kunasa na kutumia data ya kiwango cha darasani kufikiwa.

## VYANZO


1 Henry Braun, Anil Kanjee, Eric Bettinger, and Michael Kremer, *Improving Education through Assessment, Innovation, and Evaluation* (Cambridge, MA: American Academy of Arts and Sciences, 2006).

2 Barbara Bruns, Deon Filmer, and Harry Patrinos, *Making Schools Work: New Evidence on Accountability Reforms* (Washington, DC: World Bank Group, 2011); Tahir Andrabi, Jishnu Das, and Asim Ijaz Khwaja, "Delivering Education: A Pragmatic Framework for Improving Education in Low-Income Countries," World Bank Policy Research Working Paper No. 7277 (2015).

3 EFA Global Monitoring Report Team, *Education for All 2000–2015:* Achievements and Challenges (Paris: UNESCO, 2015).

4 Paul Black and Dylan Wiliam, "Classroom Assessment and Pedagogy," *Assessment in Education: Principles, Policy & Practice* 25, no. 6 (2018): 551–575.

5 Sonali Nag, Shula Chiat, Carole Torgerson, and Margaret J. Snowling, *Literacy, Foundation Learning and Assessment in Developing Countries: Final Report* (London: Department for International Development, 2014).

6 Patience Sowa, Rachel Jordan, Wendi Ralaingita, and Benjamin Piper. *Higher Grounds: Practical Guidelines for Forging Learning Pathways in Upper Primary Education* (in press).

7 Adapted by Dylan Wiliam, "Formative Assessment: Getting the Focus Right," *Educational Assessment* 11 (2011): 283–289; Michael Scriven, "The Methodology of Evaluation," in Perspectives of Curriculum Evaluation, vol. 1, edited by Ralph W. Tyler, Robert M. Gagné, and Michael Scriven (Chicago, IL: Rand McNally, 1967); Benjamin S. Bloom (ed.), *Taxonomy of Educational Objectives: Book 1, Cognitive Domain* (Montreal: Education Nouvelle, 1969).

8 Sowa et al., *Higher Grounds*; Dylan William and Paul Black, "Meanings and consequences: a basis for distinguishing formative and summative functions of assessment," *British Educational Research Journal* 22 (1996).

9 Young-Suk Grace Kim and Marcia Davidson, *Assessment to Inform Instruction: Formative Assessment* (Washington, D.C.: USAID, 2019).

10 Lant Pritchett, Rukmini Banerji, and Charles Kenny, *Schooling Is Not Education! Using Assessment to Change the Politics of Non-Learning* (Washington, DC: Center for Global Development, 2013).

11 Wiliam and Black, "Meanings and Consequences," 1996.

12 Dean Fink and Louise Stoll, "Educational Change: Easier Said Than Done," in *International Handbook of Educational Change*, edited by Andy Hargreaves, Ann Lieberman, Michael Fullan, and David Hopkins (Dordrecht: Springer, 1998).

13 H. Richard Milner IV, "Confronting Inequity/ Assessment for Equity," *Educational Leadership* 75, no. 5 (2018): 88–89; Yusuf Sayed and Anil Kanjee, "Assessment in Sub-Saharan Africa: Challenges and Prospects," *Assessment in Education: Principles, Policy & Practice* 20, no. 4 (2013): 373–384.

14 Bernard Weiner, *Achievement Motivation and Attribution Theory* (Morristown, NJ: General Learning Press, 1974).

15 Connie M. Moss and Susan M. Brookhart, *Advancing Formative Assessment in Every Classroom: A Guide for Instructional Leaders*, 2nd ed. (Alexandria, VA: Association for Supervision and Curriculum Development, 2019).

16 Linda F. Winfield, "Performance-Based Assessments: Contributor or Detractor to Equity?," in *Equity and Excellence in Educational Testing and Assessment*, edited by Michael T. Nettles and Arie L. Nettles (Dordrecht: Springer, 1995); Peter Afflerbach, Barbara Kapinus, and Marshá Taylor DeLain, "Reading Assessment: Equity and Performance-Based Assessment: An Insider's View," *Reading Teacher* 48, no. 5 (1995): 440–442.

17 Yue-Yi Hwa, Michelle Kaffenberger, and Jason Silberstein, "Aligning Levels of Instruction with Goals and the Needs of Students (ALIGNS): Varied Approaches, Common Principles," *RISE Insight Series* 2020/022 (2020).

18 Ibid.

19 Wiliam and Black, "Meanings and Consequences," 1996.

20 Maaike Christine Heitink, Fabienne van der Kleij, Bernard P. Veldkamp, et al., "A Systematic Review of Prerequisites for Implementing Assessment for Learning in Classroom Practice," *Educational Research Review* 17 (2016): 50–62.

21 Lorna Earl and Steven Katz, *Rethinking Classroom Assessment with Purpose in Mind: Assessment for Learning, Assessment as Learning, Assessment of Learning* (Winnipeg, Manitoba: Western Northern Canadian Protocol, 2006).

22 Teaching at the Right Level, "Assessment," https://www.teachingattherightlevel.org/the-tarl-approach/assessment.

23 E. M. Botha, "Turning the Tide: Creating Professional Learning Communities (PLC) to Improve Teaching Practice and Learning in South African Public Schools," *Africa Education Review* 9, no. 2 (2012): 395–411.

24 Julius Atuhurra and Michelle Kaffenberger, "System (In)Coherence: Quantifying the Alignment of Primary Education Curriculum Standards, Examinations, and Instruction in Two East African Countries," RISE Working Paper Series 20/057 (2020). Atuhurra and Kaffenberger, "System (In)Coherence," 2020.

25 World Bank Group, *Teach Observer Manual* (Washington, DC: World Bank Group, 2019).

26 Kwame Akyeampong, John Pryor, and Joseph Ghartey Ampiah, "A Vision of Successful Schooling: Ghanaian Teachers' Understandings of Learning, Teaching, and Assessment," Comparative Education 42, no. 2 (2006): 155–176.

27 John Hattie, *Visible Learning: A Synthesis of Over 800 Meta-Analyses relating to Achievement* (New York, NY: Routledge, 2009), p. 28.

28 Tangerine, "Tangerine:Teach," http://www.tangerinecentral.org/class.

29 Icek Ajzen and Martin Fishbein, *Understanding Attitudes and Predicting Social Behavior* (Englewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall, 1980).